CHUNYA TOBACCO GROWERS CO-OPERATIVE UNION LTD REG.NO.AFF-MBY-CHN-DC-2023-40
(CHUTCU LTD)
BOX 83, TEL.NO.0252520082
E-mail chutcuchunya@gmail.com

Kumb.Na.AB.31/06/02/04 30/12/2025.

## 1. TANGAZO LA MWALIKO WA ZABUNI YA UJENZI WA KITUO CHA KUUZA MAFUTA CHA CHUTCU LTD.

CHUTCU LTD ni Chama kikuu cha Ushirika cha wakulima wa mazao ambacho kinajishughulisha na usimamizi katika uzalishaji na uuzaji wa mazao ya tumbaku, mahindi na Alizeti katika Mikoa ya Mbeya na Songwe. Ni chama kilichosajiliwa tarehe 30 januari 2000 chini ya sheria ya vyama vya ushirika Na 15 ya mwaka 1991 kwa usajili wa Na 5559 na kutokana na mabadiliko ya sheria ya ushirika Na 6 ya mwaka 2013 yaliyofanyika tarehe 16 Februari 2023, CHUTCU Ltd ikasajiliwa kwa Na AFF-MBY-CHN-DC-2023-40 ikiwa katika Makao yake makuu yaliyopo mtaa wa kibaoni, Wilaya ya Chunya, mkoani mbeya, Nchini Tanzania.

## 2. KAZI YA UJENZI WA KITUO CHA MAFUTA.

Katika mwaka wa fedha 2025/2026 Chama Kikuu cha CHUTCU Ltd kimepanga kutekeleza Bajeti yake ya Maendeleo kwa kujenga kituo cha kuuza mafuta ya aina mbalimbali. Baada ya chama kukamilisha hatua ya kupata kibali cha ujenzi kilichotolewa kwa ***Kumb.Na.LA/69/209/07/114*** kutoka katika ofisi ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika Tanzania bara, Bodi ya Uongozi wa chama cha CHUTCU LTD inatoa mwaliko sasa kwa wale wote watu wenye uwezo na uzoefu na pia wenye usajili kutoka Bodi ya Usajili ya Wakandarasi (CRB) kushiriki kuomba zabuni hii muhimu ya kujenga kituo cha mafuta bila kukosa.

## 3. UKUBWA WA KITUO CHA MAFUTA.

Ni SQM 4900.

## 4. MAHALI LINAPOJENGWA.

Ghala hili litajengwa Kijiji cha Isangawana kilichopo Kata ya Matwiga Tarafa ya kipembawe, Wilaya ya Chunya Mkoani Mbeya.

CamScanner

## 5. MUDA WA UJENZI.

Muda wa ujenzi wa kituo cha mafuta hili unatarajiwa kuwa ni miaka 2 yaani kuanzia 2026 na 2027 mara tu baada ya kusaini mkataba wa kazi.

## 6. SIFA ZA MKANDARASI.

Ujenzi wa kituo cha mafuta hili utatumia njia ya Mkandarasi/Mzabuni ambapo atatakiwa kuwa na sifa zifuatazo;

i. Awe Mtanzania

ii. Lazima awe na usajili halali wa CRB Daraja la 'V' (tano) au zaidi, na awe amesajiliwa kwa kazi za majengo.

iii. Lazima awe timu ya kitaalamu yenye wataalam waliosajiliwa ( yaani Mhandisi, Msanifu majengo, Mkadiriaji Majenzi, 'site-foreman)

iv. Awe na Uzoefu katika kutekeleza miradi yenye hadhi sawa au zaidi ya kituo cha mafuta analoomba kujenga (angalau miradi isiyopungua mitatu (3) ndani ya miaka mitano (5)

v. Mwombaji awe tayari kusimamia usalama wa eneo la kazi na kwa wafanyakazi wote.

vi. Muombaji wa kazi anatakiwa kuambatanisha nyaraka zifwatazo, ripoti za ukaguzi , wasifu wa kampuni (CRB) wasifu wa wafanyakazi wa ngazi zote za utendaji, usajili wa kampuni na cheti cha kulipa kodi (TIN).

vii. Muombaji anatakiwa kuwasilisha maelezo ya Taasisi alizofanyia kazi, kwa kuonesha barua ya kupewa kazi (*letter of acceptance*) au cheti cha kukamilisha kazi (*certificate of Completion*). Nyaraka hizo ziambatanishwe kwenye barua ya maombi yake.

viii. Awe na uwezo wa kusoma/kukadiria na kutafasiri michoro, vipimo na uwiano wa vifaa vya ujenzi pamoja na gharama kwa ujenzi kwa vipengele mbalimbali kulingana ramani.

ix. Awe na uwezo wa kuwalipa mafundi na vibarua atakaowaajiri kabla ya malipo yake kufanyika, na malipo ya kazi yatafanyika mara baada ya *Mhandisi Msimamizi* kuridhika na ubora wa kazi iliyofanyika.

x. Awasilishe mpango kazi wake ukionesha mtiririko wa shughuli zote pamoja na muda atakaotumia ili kukamilisha/kuzikamilisha.

xi. Awe na Akaunti ya Benki kwa ajili ya kufanyia malipo ya kazi yake na malipo yote ya kazi yatafanyika kwa njia ya Benki.

xii. Awe na uwezo wa kufanya kazi kuanzia hatua ya awali hadi umaliziaji (*finishing*).

CamScanner

## 7. AINA YA KAZI ZITAKAZOFANYIKA.

### i. OFFICE BUILDING

a.Kufyatua tofali.

b.Kujenga msingi wa jengo kwa mawe (sub structure).

c.Kunyanyua jengo (super structure).

d.Kuezeka (roof structure and covering).

e.Kusimika fremu na kufunga milango na madirisha.

f.Umaliziaji (finishing).

g.Kuweka umeme na mifumo ya maji safi na taka awamu ya kwanza ikiwemo makaro ya maji taka kubwa na dogo.

h.Kupaka rangi na mapambo (painting na decoration).

i.Kuweka umeme na mifumo yam aji safi na taka Awamu ya pili.

j.Kuweka furniture.

k.Kufanya kazi zingine zitakazoelekezwa na Mhandisi Msimamizi.

### ii. FILL STATION CANOPY

a.Sub structure
b.Walkways
c.Off-loading
d.Frames (steel columns)
e.Steel roof structure
f.Roofing
g.Aluco bond for roof fascial and sides of the column
h.Service work
i.Installation of fuel pumps
j.Testing and commissioning of pumps

### iii. FARM TANKS.

a. Pit excavation
b. Construction of pit walls
c. Fabrication of Fuel storage tanks
d. Painting of storage tanks with tree coat red-oxide and bituminous materials
e. Installation of fuel storage tanks.
f.Testing and commissioning of storage tanks.

## 8. WAJIBU WA MUOMBAJI WA KAZI.

Mwombaji mwenye Sifa, uwezo na nia ya kuomba kazi anakaribishwa kufanya ziara ya kutembelea eneo litakalojengwa kituo cha mafuta ili kujiridhisha kwa kuona na kupata ufafanuzi zaidi jambo ambalo hajaelewa na pia kuchukua BOQ za Michoro ya kazi anayoomba katika ofisi za CHUTCU Ltd.

CamScanner

## 9. TALATIBU ZA KUTUMA MAOMBI.

Maombi yote yatapokelewa kwa njia mbili tu:

i. Tarehe ya kuanza kuchukuwa fomu/kitabu cha tenda ni 31/12/2025 muda kuanzia saa 2:00am hadi saa 10.00 pm

ii. Kuleta katika ofisi za CHUTCU Ltd zilizopo Chunya Mjini na kusaini kwenye kitabu cha waombaji wa zabuni kitakachokuwepo ofisini.

iii. Kutuma kwa njia ya barua pepe ya ofisi ambayo ni chutcuchunya@gmail.com

iv. Barua za Maombi zote zielekezwe kwa;

**MENEJA MKUU,**
**CHUTCU LTD,**
**S.L.P 83,**
**CHUNYA.**

## 10. ADA YA MAOMBI.

Waombaji wote wanatakiwa kulipa ada ya **TZS 300,000.00** kupitia Akaunti Namba: **01J1066308000** yenye Jina la ***Chunya Tobacco Growers cooperative Union*** iliyopo Benki ya CRDB kabla ya kuchukua BOQ na Fedha hiyo haitarudishwa kwa mtu yeyote ambaye atashindwa au kushinda katika ushindani wa zabuni iliyotangazwa.

## 11. MWISHO WA KUWASILISHA MAOMBI.

Mwisho wa kuwasilisha Maombi ya zabuni ni siku ya **JUMATANO TAREHE 14 JANUARI 2026 SAA 10:00 JIONI/ALASIRI.** Na muombaji atakayechelewa kuwasilisha maombi yake tarehe, siku na muda ulioainishwa maombi yake hayatapokelewa na kushughulikiwa na kamati ya kufungua zabuni. Aidha, ufunguzi wa zabuni utafanyika siku ya **IJUMAA TAREHE 16/01/2026 MUDA UTAKUWA NI SAA 4:00 ASUBUHI.** Hivyo waombaji au wawakilishi wote wanakaribishwa kuhudhuria ufunguzi wa maombi yao katika ukumbi wa CHUTCU LTD.

CHUNYA TOBACCO GROWERS COOPERATIVE UNION LTD
REG NO , 5559
P. O. Box 83
CHUNYA

**SEBASTIAN M. MASIKA**
**MWENYEKITI WA BODI**
**CHUTCU LTD.**